

SERA

Sera ya Ustahiki wa Kupata Usaidizi wa Kifedha

Sera Hii Inatumika katika maeneo yafuatayo ya Corewell Health:

Beaumont Corporate Shared Services, Beaumont Dearborn, Beaumont Farmington Hills, Beaumont Grosse Pointe, Beaumont Medical Group, Beaumont Pharmacy Solutions, Beaumont Royal Oak, Beaumont Taylor, Beaumont Trenton, Beaumont Troy, Beaumont Wayne, Big Rapids (Mecosta County Medical Center), Continuing Care, Corewell Health Watervliet Hospital, Corporate (Spectrum Health System), Gerber Memorial (Newaygo County General Hospital Association), Ludington (Memorial Medical Center of West Michigan), Outpatient/Physician Practices, Pennock (Pennock Hospital), Post Acute Care (Beaumont), Reed City (Reed City Hospital Corporation), SH GR Hospitals (Spectrum Health Hospitals), SHMG, Spectrum Health Lakeland (Lakeland Hospitals at Niles and St. Joseph Inc.; Applicable Corewell Health South Regional Sites), United/Kelsey (Spectrum Health United; Spectrum Health Kelsey Hospital), Zeeland (Zeeland Community Hospital)

Matumizi Yanakomea kwa:	N/A
Nambari ya Marejeleo:	2983
Nambari ya Toleo:	11
Tarehe ya Kutekelezwa:	11/01/2022
Eneo la Utendaji:	Fedha, Ufikiaji wa Wagonjwa
Eneo la Idara:	Fedha, Kipindi cha Mapato

Ilani ya Kutobagua: Corewell Health na kampuni zake zote tanzu zinapaswa kutoa huduma bora za afya kwa watu wote, kwa mujibu wa sera yake. Corewell Health haitabagua kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, uraia, jinsia, dini, umri, ulemavu, imani za kisiasa, mwelekeo wa ngono, hali ya ndoa au familia. Maamuzi ya kusajiliwa na matibabu yatalingana kimahususi na mahitaji ya kimatibabu ya mgonjwa na uwezo wa hospitali kutoa huduma za matibabu na za kiafya zinazohitajika. Hutakatazwa kujisajili wala kupata matibabu kwa misingi ya kabila, rangi, jinsia, ngono, mbari, asili ya nchi, dini, ulemavu, umri, hali ya HIV, hali ya uanajeshi, chanzo cha malipo ya huduma au kwa misingi mingine yoyote iliyopigwa marufuku na sheria za serikali, za jimbo au za kimaeneo. Wagonjwa watatibiwa kulingana na utambulisho wa jinsia yao. Aidha, maeneo yaliyoidhinishwa ya National Health Service Corps (“NHSC”) na Michigan State Loan Repayment Program (“MSLRP”) hayatabagua katika kutoa huduma kwa mtu binafsi (na hayatategemea ustahiki kwenye mpango) kwa msingi wa uwezo wa mtu wa kulipa, iwe malipo ya huduma hizo yatafanywa kupitia Medicare, Medicaid, au CHIP; na hayatabagua kwa misingi ya mbari, rangi, jinsia, asili ya nchi, ulemavu, dini, umri, mwelekeo wa ngono au utambulisho wa jinsia ya mtu. Angalia sera ya [Haki na Wajibu wa Mgonjwa](#) (Corewell Health Southeast Michigan), [Haki na Wajibu wa Mgonjwa](#) (Corewell Health Southwest Michigan), au [Haki na Wajibu wa Mgonjwa](#) (Corewell Health West Michigan) ili upate maelezo zaidi.

Sera ya mpango wa punguzo maalum inatumika katika maeneo yaliyoidhinishwa ya NHSC na MSLRP pekee. Angalia [Kiambatisho cha B](#).

Angalia [Kiambatisho cha C](#) ili upate ilani kamili ya kutobagua na pia upatikanaji wa usaidizi katika lugha mbalimbali.

1. Madhumuni

Kubainisha mchakato wa kufanya uamuzi unaofaa wa anayestahiki kupokea usaidizi wa kifedha katika Corewell Health. Kutoa taarifa kuhusu upatikanaji wa usaidizi wa kifedha kwa wagonjwa na kwa umma na kuhakikisha mwongozo usiobadilika unatumika kwa maombi ya usaidizi wa kifedha, bila kujali eneo la Corewell Health ambako huduma za wagonjwa zinatolewa.

Sera hii inalenga kutimiza masharti ya Kifungu cha 501(r) cha Kanuni ya Ndani ya Mapato ya 1986, jinsi ilivyorekebishwa, ambayo inatoa masharti fulani kwa hospitali kuhusu usaidizi wa kifedha, vikomo vya kutozwa, na shughuli za malipo na ukusanyaji. Wagonjwa ambao hawana njia ya kulipia huduma inayotolewa katika maeneo ya Corewell Health wanaweza kuomba usaidizi wa kifedha, na wanaweza kupewa usaidizi wa kifedha, kwa mujibu wa sheria na masharti ya sera hii.

Sera hii pia inalenga kutimiza kanuni fulani za kuripoti gharama za Medicare.

2. Majukumu

Sera Hii ya Ustahiki wa Usaidizi wa Kifedha kwenye Corewell Health (“Sera”) itatekelezwa na wataalamu wateule wa Corewell Health kama ilivyobainishwa katika elimu na michakato ya idara husika ya ustahiki wa usaidizi wa kifedha.

3. Maudhui ya Sera

Corewell Health itaondoa wajibu wa kifedha wa mgonjwa kwenye huduma za Dharura au Zinzohitaji Matibabu katika hali ambapo mgonjwa au mdhamini anatimiza masharti ya chini ya mwongozo wa ugumu wa kifedha, yaliyobainishwa katika Kifungu cha 6.6 hapa chini, na anashirikiana na Corewell Health katika utelekezaji wa michakato yake ya idara ya ustahiki wa usaidizi wa kifedha. Lazima ubainishaji wa nia njema ya usaidizi wa kifedha ufanyike kabla ya kuondolewa kwa gharama zozote.

4. Falsafa

Huduma za Dharura na Zinzohitaji Matibabu zitakuwa misingi ya matibabu, wala si wajibu wa kifedha. Uamuzi wa usaidizi wa kifedha utatolewa kulingana na mahitaji ya kifedha yanayoweza kuthibitishwa na utatolewa kwa kushirikiana na mgonjwa au mdhamini panapowezekana. Wagonjwa au wadhamini wote wanaotuma ombi la usaidizi wa kifedha watapitia mchakato sawa wa usaidizi wa kifedha bila kujali mdhamini mkuu.

Huduma Inayohitaji Matibabu hufafanuliwa kuwa huduma zinazohitajika ili kutambua au kutibu ugonjwa au jeraha ambalo limebainishwa au linalokisiwa kuwa Linahitaji Matibabu kwa kuzingatia kiwango kinachofaa zaidi cha matibabu. Kulingana na hali ya matibabu ya mgonjwa, mazingira yanayofaa zaidi ya kutoa huduma za matibabu yanaweza kuwa nyumbani, ofisi ya daktari, hospitali ya wagonjwa wa kutwa, au matibabu ya muda mrefu, maeneo ya kurekebisha tabia au kitanda cha hospitali. Ili huduma ibainishwe kuwa Inahitaji Matibabu, lazima:

- Itakiwe kutibu ugonjwa au jeraha;
- lendane na utambuzi na matibabu ya hali za mgonjwa;
- lilingane na viwango vya mbinu bora za matibabu;
- Isiwe kwa faida ya mgonjwa au daktari wa mgonjwa; na
- Iwe katika kiwango cha huduma kinachofaa zaidi mgonjwa kama ilivyobainishwa na hali ya matibabu ya mgonjwa, wala si hali ya familia au hali ya kifedha ya mgonjwa

Huduma ya Dharura huchukuliwa kuwa “Inayohitaji Matibabu.”

5. Sera ya Huduma ya Matibabu ya Dharura

Corewell Health itatoa huduma, bila ubaguzi, katika hali za matibabu ya dharura kwa watu bila kujali uwezo wao wa kulipa au ustahiki wa kupata usaidizi wa kifedha. Hali za matibabu ya dharura zinaweza kutokana na kuanza kwa ghafla kwa hali ya matibabu yenye dalili kali ambazo, bila usaidizi wa matibabu mara moja, zinaweza kuhatarisha afya ya mgonjwa, kusababisha kuathirika kwa utendaji wa kiungo chochote cha mwili kikamilifu au kwa kiasi fulani. Corewell Health haitahusika katika vitendo vinavyowakataza watu kutafuta huduma za matibabu ya dharura, na,

kwa hali hiyo, huduma ya Dharura itatolewa bila kuathiriwa na ukusanyaji wa madeni au madai ya kulipia huduma za matibabu mapema kama ilivyofafanuliwa katika Sera ya [Matibabu ya Dharura na Machungu ya Uzazi \(EMTALA\)](#) (Corewell Health Southeast Michigan) au Sera ya [Hali za Matibabu ya Dharura / Sera ya Uhamishaji \(MATIBABU YA DHARURA NA MACHUNGU YA UZAZI - EMTALA\)](#) (Corewell Health Southwest and West Michigan).

6. Sera

6.1. Masharti ya Makazi

Ili kudumisha lengo letu la kuboresha afya, kuendeleza utu, na kuleta tumaini, Corewell Health itadhibiti watu wanaozingatiwa kupata usaidizi wa kifedha kuwa wanaotuma maombi ambao wanaonyesha kuwa wameishi ndani ya Jimbo la Michigan kwa kipindi kisichopungua miezi sita au katika jumuiya ambayo imejumuishwa katika tathmini ya mahitaji ya afya ya jumuiya kwenye hospitali kama “jumuiya” inayohudumia. Kanuni hiyo inaweza kubadilishwa kwa wagonjwa wanaohitaji huduma za Dharura au wale wanaotafuta huduma inayohitaji Matibabu ambayo haipatikani ndani ya eneo la huduma ya wengine.

6.2. Muhtasari

- 6.2.1.** Kabla ya kuomba usaidizi wa kifedha, mgonjwa au mdhamini na Corewell Health watajaribu njia zote nyingine za malipo kama ilivyofafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 6.3.
- 6.2.2.** Sera ya Corewell Health inataka suluhu ya malipo kwa huduma isiyo ya Dharura au Isiyohitaji Matibabu, ikiwa ni pamoja na lakini si tu, utafiti au majaribio, huduma za mapambo ya hiari na taratibu za upasuaji kutokana na ubonge *kabla* ya huduma au wakati taarifa itatolewa kwanza, isipokuwa mipango mingine iliyoidhinishwa ya malipo iwe imewekwa. Corewell Health pia itataka suluhu ya malipo kwa huduma isiyo ya Dharura ambayo haijaidhinishwa au kulindwa kwa bima.
- 6.2.3.** Wagonjwa au wadhamini wanaobaini kuwa hawawezi kulipa au wamebainishwa na Corewell Health kuwa huenda hawawezi kulipia huduma, wataelekezwa kwa wataalamu wateule wa Corewell Health kwa ajili ya ukaguzi, panapohitajika. Wafanyakazi wa Corewell Health wanaweza kuendelea kukagua maombi ya usaidizi wa kifedha ili kubaini iwapo kuna uwezo kutolipa umethibitishwa. Mgonjwa au mdhamini anaweza kuombwa kukamilisha ombi la usaidizi wa kifedha. Ripoti ya mikopo inaweza kutumiwa ili kuthibitisha maelezo yaliyotolewa kwenye ombi lakini haitatumikiwa kimahususi kubainisha ustahiki wa usaidizi wa kifedha. Sehemu ya mchakato au mchakato wote wa kutuma ombi la fedha inaweza kuondolewa kwa wagonjwa au wadhamini fulani ambao wanatimiza masharti ya kupata usaidizi wa kifedha na wamethibitishwa, kwa mujibu wa sera na taratibu za Corewell Health. Wakati wa mchakato wa kukagua ustahiki wa kukisiwa, Corewell Health inaweza kukadiria mapato ya familia ya mgonjwa kwa kutumia muundo wa hesabu uliobuniwa na washirika wengine, ambao hutumia maelezo ya ripoti ya mikopo, data inayoripotiwa na mtumiaji mwenyewe, vyanzo vya data za utangazaji na mapato ya wastani kwa wengine walio karibu na anwani iliyoripotiwa ya mgonjwa. Mifano mingine ya ustahiki wa kukisia inaweza kujumuisha watu ambao wamebainishwa kuwa hawana makao.
- 6.2.4.** Iwapo, kutokana na mchakato wa kutuma ombi la kifedha, vigezo vya usaidizi wa kifedha havijtamizwa, mgonjwa au mdhamini atashauriwa kupanga malipo kwa mujibu wa [Sera ya Malipo na Ukusanyaji](#) (Corewell Health Southeast Michigan) au [Sera ya Malipo na Ukusanyaji wa Pesa Anazodaiwa Mgonjwa Husika](#) (Corewell Health Southwest and West Michigan) na taratibu zinazotumika, ambapo mgonjwa au mdhamini anaweza kustahiki kupata mapunguzo na/au chaguo nyingine za malipo kama vile mapunguzo ya malipo ya mapema, mipango ya malipo nk.
- 6.2.5.** Ikionekana kuwa mwongozo wa ugumu wa fedha unaweza kutumika, mgonjwa au mdhamini anaweza kuombwa kutoa hati zinazothibitisha kama ilivyobainishwa katika ombi, na ombi hilo litachakatwa ipasavyo.
- 6.2.6.** Akaunti ya mgonjwa itapokea hati ya matokeo ya uamuzi. Juhudi muhimu zitafanywa ili kumwarifu mgonjwa/mdhamini kwa kuandika kuhusu uamuzi (ikiwa ni pamoja na, panapohitajika, usaidizi ambao mtu huyo anastahiki) na misingi ya uamuzi.

Huluki zitarejelea Hati husika zilizo katika hati hii panapohitajika
Huenda machapisho ya hati hii hayazingatii tarehe na yanayapaswa kuchukuliwa kuwa yasiyodhibitiwa.

6.2.7. Hati zote zinazotumika na zinazohitishwa maombi zitahifadhiwa kwa mujibu wa [Sera na Taratibu za Kuhifadhi Hati](#) (Corewell Health Southeast Michigan) au [Sera ya Kuhifadhi, Kuharibu na Kusimamia Rekodi](#) (Corewell Health Southwest and West Michigan).

6.3. Vyanzo vya Malipo vya Washirika Wengine

Kabla ya kuomba usaidizi wa kifedha, mgonjwa au mdhamini na Corewell Health watajaribu njia zote za malipo za washirika wengine ikiwa ni pamoja na lakini si tu, Medicaid na usajili katika Health Insurance Marketplace.

Corewell Health ina haki ya kuchunguza, kuthibitisha, kuhoji na kuomba kukabidhiwa kwa:

- Manufaa yote kutoka kwa chanzo chochote cha bima ya washirika wengine;
- Manufaa yote kutoka kwenye mipango ya jimbo au serikali ambayo huenda mgonjwa au mdhamini anastahiki;
- Manufaa yote kutoka kwa shirika lolote la misaada; na/au
- Madai ya mahakamani yanayosubiri kushughulikiwa.

Usaidizi wa kifedha ndiyo suluhu ya mwisho ya utatuzi wa akaunti. Kwa hivyo, mgonjwa au mdhamini lazima atimize majukumu yote chini ya mipango yoyote inayotumika iliyo hapa juu au atumie nyenzo za kibinafsi zinazopatikana kabla ya kustahiki kupata usaidizi wa kifedha. Mgonjwa au mdhamini akishindwa kutoa maelezo yaliyoombwa au kushiriki katika mojawapo ya mipango iliyo hapo juu, anaweza kukosa usaidizi wa kifedha.

6.4. Upatikanaji wa Usaidizi wa Kifedha

Corewell Health imetekeleza hatua za kutangaza hadharani kwa wagonjwa na umma kuhusu upatikanaji wa usaidizi wa kifedha. Mbinu za mawasiliano ni pamoja, na lakini si tu, mabango katika idara ya dharura ya kila hospitali, maeneo ya usajili na maeneo mengine ya umma, na pia maelezo kwenye tovuti ya Corewell Health (kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 6.5). Isitoshe, Corewell Health itatoa muhtasari katika lugha ya kawaida kuhusu Sera ya Ustahiki wa Kupata Usaidizi wa Kifedha kama sehemu ya mchakato wa kusajili na/au kumruhusu mgonjwa aende nyumbani, na pia kuwapa watu usaidizi katika mchakato wa kutuma ombi.

Wagonjwa wataarifiwa kuhusu Sera ya Ustahiki wa Kupata Usaidizi wa Kifedha kwa kipindi cha angalau siku 120 kuanzia tarehe ya taarifa ya kwanza ya malipo baada ya mgonjwa kuondoka hospitalini. Masalio ya pesa za mgonjwa yatatumiwa kutathmini usaidizi wa kifedha kwa angalau siku 240 kuanzia tarehe ya taarifa ya kwanza ya malipo baada ya mgonjwa kuondoka hospitalini ("Kipindi cha Kutuma Ombi"). Iwapo Corewell Health itapokea ombi la usaidizi wa kifedha wakati wa Kipindi cha Kutuma Ombi, iwe ombi limekamilika au halijakamilika, itaahirisha juhudi zozote za ukusanyaji hadi uamuzi kuhusu ustahiki wa kupata usaidizi wa kifedha ufanywe.

Baadhi ya huduma zinaweza kutolewa kwa wagonjwa katika Corewell Health na watoa huduma ambao huenda wasitumie mchakato na Sera ya Corewell Health ya Ustahiki wa Kupata Usaidizi wa Kifedha. Ili uone orodha ya watoa huduma hawa, tafadhali angalia toleo jipya zaidi la [Kiambatisho cha A](#), ambacho kitasasishwa mara kwa mara maelezo yanapobadilika kadri muda unavyosonga.

6.5. Mchakato wa Utambulisho na Ombi la Usaidizi wa Kifedha

Lengo la mchakato wa ustahiki wa kupata usaidizi wa kifedha ni kubaini uwezo wa mgonjwa au mdhamini wa kulipa.

Nakala isiyolipishwa ya Sera ya Ustahiki wa Kupata Usaidizi wa Kifedha, na pia ombi la sasa la kupata usaidizi wa kifedha na muhtasari wa sera katika lugha ya kawaida, vinapatikana katika maeneo yote ya Corewell Health. Pia, nakala isiyolipishwa inaweza kupatikana katika:

- Kwa Corewell Health Southeast Michigan:
 - <https://www.beaumont.org/patients-families/billing/financial-assistance>
 - kwa kupiga simu kwa (877) 687-7309
 - au kutuma barua pepe kwa EastFinancialCounseling@corewellhealth.org
- Kwa Corewell Health Southwest Michigan:
 - <https://www.spectrumhealthlakeland.org/patient-visitor-guide/patient/billing/financial-assistance>
 - kwa kupiga simu kwa (844) 408.4103
 - au kutuma barua pepe kwa SHLFinancialCounseling@corewellhealth.org
- Kwa Corewell Health West Michigan:
 - <https://www.spectrumhealth.org/billing/financial-assistance>
 - kwa kupiga simu kwa (844) 838.3115
 - au kutuma barua pepe kwa FinancialCounseling@corewellhealth.org

Huenda kila mtu akatakiwa kukamilisha ombi la usaidizi wa kifedha na kutoa maelezo ambayo Corewell Health imeomba kama sehemu ya kutuma ombi. Corewell Health hubaini usaidizi wa kifedha kulingana na mwongozo wa ugumu wa kifedha katika Kifungu cha 6.6. Huenda Corewell Health ikataka nakala za hati ya mshahara, ripoti za kodi ya mapato ya serikali na vyanzo vingine vya mapato na uthibitishaji wa mali jinsi ilivyofafanuliwa katika ombi. Teknolojia na rekodi nyingine za umma kama vile rekodi za kufilisika, rekodi za vifo na ripoti za mirathi zinaweza kutumiwa kusaidia katika kutambua mapema na ipasavyo wagonjwa wanaostahiki kupata usaidizi, wakati hawawezi kuwasilisha maelezo kamili ya ombi, au kufanya mchakato wa kupata data inayohitajika uwe wa kiotomatiki na uchanganuzi wa uwezo wa kulipa katika hali mahususi. Wakati teknolojia inatumiwa kusaidia kukisia ustahiki, itatumika kupata maelezo yaliyoombwa kama sehemu ya ombi. Ustahiki wa kukisiwa utatolewa kwa waliotuma maombi, walio na ulinzi uliothibitishwa wa kufilisika, na wale wasio na makao kama ilivyo katika rekodi za makazi au vyanzo vingine vinavyokubalika. Huenda wanaotuma maombi wakaombwa kusaidia na kushirikiana katika kutuma maombi ya manufaa kutoka kwa bima za washirika wengine, jimbo, serikali au mipango mingine ya misaada ambayo ilitajwa awali katika Kifungu cha 6.3 hapo juu.

Mgonjwa ambaye anatumia Medicaid atakisiwa kustahiki usaidizi wa kifedha wa 100% kwa njia ya marekebisho ya huduma ya misaada.

Corewell Health inaweza kukabidhi shughuli ya kubaini ustahiki wa kupata usaidizi wa kifedha kwa kampuni za washirika katika juhudi za kuepuka urudufishaji wa shughuli. Kampuni za washirika zitakazotumia mwongozo wa sera hii kwa madhumuni ya kubaini ustahiki, kwa kulingana na idadi ya watu wanaohudumiwa, zitakuwa zimetimiza masharti ya msingi ya ombi letu. Wakati kukabidhi, Corewell Health itakagua mara kwa mara hati ya kubaini mashirika ili kuhakikisha kuwa yanatii sera hii.

6.6. Masharti ya Mwongozo wa Ugumu wa Kifedha

Isipokuwa wagonjwa wanaopokea huduma katika eneo lililoidhinishwa National Health Service Corps ("NHSC") au eneo lililoidhinishwa la Michigan State Loan Repayment Program ("MSLRP"), katika kubainisha ustahiki wa kupata usaidizi wa kifedha, Corewell Health itatathmini uwezo wa mgonjwa au mdhamini wa kulipa Corewell Health kwa huduma zinazoombwa au zilizotolewa awali.

Corewell Health itakagua maelezo kama yaliyo hapa chini wakati wa kutathmini uwezo wa kulipa:

- Viwango vya mapato
- Jumla ya mali
- Hali ya ajira
- Majukumu mengine ya kifedha
- Kiasi na mara za kulipwa kwa bili za huduma ya afya

Ripoti ya mikopo inaweza kutumiwa ili kuthibitisha maelezo yaliyo hapo juu. Corewell Health itatumia toleo la sasa la Mwongozo wa Serikali ya Marekani wa Kubaini Umaskini (FPG) kama msingi wa masharti ya ustahiki wa mapato.

Mapato yanayostahiki kwa uondoaji wa dhima zote za kifedha (huduma bila malipo) kwa pesa zinazodaiwa vinginevyo yatakuwa 250% ya kiwango cha umaskini kama ilivyofafanuliwa na FPG ya sasa (angalia <https://aspe.hhs.gov/poverty-guidelines> ili uone mwongozo wa sasa) jinsi unavyochapishwa kila mwaka na Idadi ya Huduma za Afya na Binadamu.

Rekodi za kifedha zinazohusu mapato ya familia ya mgonjwa au mdhamini zinaweza pia kuombwa, si ili kukabidhi jukumu kwa shirika lingine, lakini ili kubaini jinsi zinavyoathiri moja kwa moja hali ya kifedha ya anayetuma ombi. Familia, kama ilivyofafanuliwa na United States Census Bureau, ni kundi la watu wawili au zaidi la wanaohusiana kifamilia, iwe kupitia kuzaliwa, ndoa, kuasiliwa, au vinginevyo, wanaoishi pamoja (wasiohusiana, kama vile wanaokaa pamoja, hawajumuishwi); watu wote wanaohusiana wanaoishi katika nyumba moja wanachukuliwa kuwa watu wa familia moja. Corewell Health haizingatii watu wanaoishi katika nyumba moja, lakini wanaojitegemea kivyao, kama familia iliyojumuishwa. Hali ya makao ya muda mfupi kutokana na matibabu pia haitajumuishwa.

Historia ya matibabu ya mgonjwa, ya tabia na/au ya jamii haitazingatiwa katika kutathmini uwezo wa kulipa.

6.7. Usawa

Ili kuhakikisha utelekezaji sawa wa sera hii ndani ya Corewell Health, yafuatayo yanatumika katika maeneo yote ya Corewell Health:

- Utozaji wote utarekodiwa kwenye akaunti ya mgonjwa kwa mujibu wa taratibu za kawaida za utozaji. Ingawa utozaji ndio msingi wa madhumuni ya kuhifadhi rekodi za malipo na za ukusanyaji, gharama (wala si utozaji), ndizo zitakuwa kitengo cha msingi cha kuripoti cha kutathmini usaidizi wa kifedha.
- Huduma “hazitapunguzwa” kwa ada ya chini.
- “Heshima ya kikazi” haitatumika.
- Corewell Health haitabagua kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, uraia, jinsia, dini, umri, ulemavu, imani za kisiasa, mwelekeo wa ngono, hali ya ndoa au familia.
- Wagonjwa wanaotimiza masharti ya sera hii na ambao wameidhinishwa kupata usaidizi wa kifedha watastahiki kupata Huduma za Dharura na Zinazohitaji Matibabu bila malipo wakati wa kipindi cha kuidhinisha kilichobainishwa katika Kifungu cha 6.9. Kwa sababu Corewell Health haitozi pesa zozote kwa wagonjwa wanaostahiki kupata usaidizi wa kifedha chini ya sera hii, Corewell Health inatii kikamilifu “pesa zilizotozwa kwa jumla” na masharti ya chini ya utozaji wa jumla yatakayotumika kwenye hospitali za misaada.

6.8. Mchakato wa Kuidhinisha Maombi

6.8.1. Lazima uamuzi wote wa usaidizi wa kifedha uidhinishwe na watu wanaofaa kama ilivyobainishwa katika elimu na michakato ya idara ya ustahiki wa kupata usaidizi wa kifedha.

6.8.2. Hati husika zinapaswa kuambatana na uamuzi wote wa usaidizi wa kifedha na kuhifadhiwa kama ilivyorejelewa katika Kifungu cha 6.2.7 hapa juu.

6.9. Kipindi cha Kuidhinisha

Uidhinishaji wote wa maombi ya usaidizi wa kifedha unaofanywa chini ya Sera ya Ustahiki wa Usaidizi wa Kifedha unaweza kutekelezwa kwa kipindi cha angalau siku 90 na unajumuisha huduma husika ya Dharura au Inayohitaji Matibabu. Mabadiliko katika hali ya kifedha au ustahiki wa ziada wa mlipaji mwingine unaweza kuathiri kipindi cha kuidhinisha na kutaka ukaguzi wa ziada.

6.10. Mchakato wa Kukata Rufaa

Watu ambao wamezuiwa kupata usaidizi wa kifedha chini ya masharti ya Sera hii wanaweza kuomba ukaguzi wa uamuzi. Ukaguzi utafanyika katika kiwango kinachofuata cha mamlaka ya uidhinishaji.

Rufaa zinazoendelea juu ya kiwango cha usimamizi ndani ya Patient Access huwasilishwa kwenye jopo la viongozi wakuu wa Corewell Health waliochaguliwa na Corewell Health SVP of Revenue Cycle au mwakilishi wake.

6.11. Juhudi za Ukusanyaji katika Tukio la Kukosa Kulipa

Katika tukio ambapo mgonjwa au mdhamini hatumi ombi wala kustahiki kupata usaidizi chini ya Sera hii, vitendo vya ukusanyaji ambavyo Corewell Health inaweza kuchukua katika tukio la kushindwa kulipa vimefafanuliwa kikamilifu zaidi katika sera zilizoordheshwa hapa chini:

- [Sera ya Malipo na Ukusanyaji](#) (Corewell Health Southeast Michigan).
- [Sera ya Malipo na Ukusanyaji kwa Salio la Mgonjwa Husika](#) (Corewell Health Southwest and West Michigan).

Nakala isiyolipishwa ya sera zilizo hapo juu zinaweza kupatikana katika:

- Kwa Corewell Health Southeast Michigan:
 - <https://www.beaumont.org/patients-families/billing/financial-assistance>
 - kwa kupiga simu kwa (877) 687-7309
 - au kutuma barua pepe kwa EastFinancialCounseling@corewellhealth.org
- Kwa Corewell Health Southwest Michigan:
 - <https://www.spectrumhealthlakeland.org/patient-visitor-guide/patient/billing/financial-assistance>
 - kwa kupiga simu kwa (844) 408.4103
 - au kutuma barua pepe kwa SHLFinancialCounseling@corewellhealth.org
- Kwa Corewell Health West Michigan:
 - <https://www.spectrumhealth.org/billing/financial-assistance>
 - kwa kupiga simu kwa (844) 838.3115
 - au kutuma barua pepe kwa FinancialCounseling@corewellhealth.org

Ilani tofauti iliyoandikwa itatolewa kwa kila mtu angalau siku 30 kabla ya vitendo vyovyote ya ukusanyaji kuanzishwa.

6.12. Misingi ya Kuhesabu Jumla ya Utozaji (AGB)

Corewell Health (yakiwemo mashirika yanayohusiana) haitozi wagonjwa wanaostahiki kwa mujibu wa Sera ya Usaidizi wa Kifedha ("FAP") kwa huduma za Dharura na Zinazohitaji Matibabu, kando na pesa za utozaji wa jumla (AGB) kwa wale wanaolindwa kwa bima inayoshughulikia huduma hiyo. Badala yake, Corewell Health inatoa huduma za Dharura na Zinazohitaji Matibabu bila malipo kwa wagonjwa wowote wanaotimiza masharti ya kupata usaidizi wa kifedha chini ya Sera hii. Corewell Health hutumia mbinu ya kukagua nyuma na huhesabu asilimia ya AGB kwa kila hospitali kwa kugawanya jumla ya kiasi chote kinachodaiwa kutokana na huduma za Dharura na Zinazohitaji Matibabu ambazo zimeruhusiwa kwenye Medicare bila malipo, pamoja na bima ya binafsi ya miezi kumi na miwili (12), na jumla ya utozaji wa madai hayo. Corewell Health huchapisha nakala ya sasa ya asilimia na maelezo ya hesabu ya AGB kwenye tovuti yake:

- [billing-percentages-english.pdf \(beaumont.org\)](#) (Corewell Health Southeast Michigan)
- [Amounts-generally-bill-agb-table2019-english.pdf \(spectrumhealthlakeland.org\)](#) (Corewell Health Southwest Michigan).
- [spectrum-health-amounts-generally-billed-table.pdf \(contentstack.io\)](#) (Corewell Health West Michigan).

Kwa mujibu wa sheria ya Michigan, Corewell Health haitatoza mgonjwa ambaye hana bima aliye na mapato ya familia yasiyozidi 250% ya FPG, zaidi ya 115% ya kiwango cha malipo ya Medicare.

6.13. Mzigo Mkubwa Zaidi wa Kifedha

Corewell Health inatambua kuwa matukio mabaya ya afya yanaweza kusababisha mzigo mkubwa zaidi wa kifedha kwa mgonjwa na familia, kwa hivyo, Corewell Health inahifadhi haki ya kukagua hali mbaya zaidi kulingana na mtu binafsi. Uamuzi wa punguzo la wajibu wa kifedha utafanywa kwa kuzingatia bili za matibabu zilizojumlishwa ndani ya siku 240 zilizopita, na pia zinazokisiwa kutokea ndani ya siku 90 zijazo. Mzigo mzito zaidi wa kifedha ni ule unaosababisha mzigo wa 25% ya mapato ya familia ya mwaka au zaidi.

7. Marekebisho

Corewell Health inahifadhi haki ya kubadilisha, kubatilisha, kugeuza au kuondoa sera hii wakati wowote bila ilani ya awali iliyoandikwa.

Mabadiliko yoyote kwenye sera hii yanakabidhiwa kwa Rais na Afisa Mkuu Mtendaji wa Corewell Health na wajumbe wake. Marekebisho yote kwa viambatisho vyovyote vya sera hii na hati za uthibitishaji zinazohusiana na sera hii, kama vile ombi la usaidizi wa kifedha, muhtasari wa lugha ya kawaida, nk., vimekabidhiwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa Usajili na Ushauri wa Kifedha, Corewell Health.

8. Sera Zinazobadilishwa:

Sera hii inachukua nafasi ya sera zifuatazo kuanzia tarehe ya kutekelezwa kwa Sera ya Ustahiki wa Kupata Usaidizi wa Kifedha katika Spectrum Health Hospital Group Financial Assistance Eligibility Policy #SH-ADMIN-FIN-001; Lakeland Health Financial Assistance Policy CORP #176; Spectrum Health Financial Assistance Eligibility Policy #2983; Beaumont Health Financial Assistance Policy #9349605.

9. Marejeleo

[Haki na Majukumu ya Mgonjwa](#) (Corewell Health Southeast Michigan)
[Haki na Majukumu ya Mgonjwa](#) (Corewell Health Southwest Michigan)
[Haki na Majukumu ya Mgonjwa](#) (Corewell Health West Michigan)
[Sera ya Malipo na Ukusanyaji](#) (Corewell Health Southeast Michigan)
[Malipo ya Salio la Mgonjwa na Sera ya Ukusanyaji](#) (Corewell Health Southwest and West Michigan)
[Sheria ya Matibabu ya Dharura na Machungu ya Uzazi \(EMTALA\)](#) (Corewell Health Southeast Michigan)
[Sera ya Hali ya Dharura ya Matibabu / Matibabu/ Uhamishaji \(MATIBABU YA DHARURA NA MACHUNGU YA UZAZI - EMTALA\)](#) (Corewell Health Southwest and West Michigan)
[Sera na Taratibu za Kuhifadhi Hati](#) (Corewell Health Southeast Michigan)
[Sera ya Kuharibu, Kuhifadhi na Kusimamia Rekodi](#) (Corewell Health Southwest and West Michigan)

10. Kubuni na Kuidhinisha Sera

Mmiliki wa Hati:

Kyleigh Hafeli (Project Specialist)

Mwaandishi au Waandishi:

Sarah Clark (VP, Registration/Fin Counseling)

Mkaguzi au Wakaguzi:

Amy Assenmacher (SVP, Finance Revenue Cycle), Benjamin Schwartz (President, Corewell Health East), Celeste McIntyre (SVP, Corporate Controller), Christopher Flores (SVP, Finance), Courtney Guernsey (VP, Patient Financial Services), Darryl Elmouchi (Chief Operating Officer), Hardik Dalal (SVP, Finance), Loren Hamel (President, Corewell Health South), Matthew Cox (Chief Financial Officer), Steffany Dunker (SHWM Volunteer)

Mwidhinishaji:

Christina Freese Decker (President & CEO)

11. Maneno Muhimu:

Usaidizi, Umaskini, Ustahiki, Misaada, suluhu, Heshima ya kikazi, huduma ya misaada, huduma bila malipo, fap

Sera ya Ustahiki wa Kupata Usaidizi wa Kifedha kwenye Corewell Health- Kiambatisho cha A

Sera ya Ustahiki wa Kupata Usaidizi wa Kifedha kwenye Corewell Health (“Sera”) inashughulikia tu Huluki za Corewell Health (zilizoordheshwa katika Sera hii) na watoa huduma wote walioajiriwa na Huluki hizi.

Corewell Health Southeast Michigan:

Orodha ya watoa huduma ambao hawashughulikiwi na Sera hii inaweza kusomwa kwenye tovuti yetu kwa kubofya [hapa](#).

Corewell Health Southwest Michigan:

Sera hii haitumiki kwenye Caring Circle. Orodha ya watoa huduma ambao hawajashughulikiwa na sera hii inaweza kuonekana kwenye tovuti yetu kwa kubofya [hapa](#).

Corewell Health West Michigan:

Orodha ya watoa huduma ambao hawajashughulikiwa na sera hii inaweza kuonekana kwenye tovuti yetu kwa kubofya [hapa](#).

Mpango wa Punguzo Maalum wa National Health Service Corps na Michigan State Loan Repayment - Kiambatisho cha B

Yafuatayo yatumika tu kwa Tovuti Za Majaribio Zilizoidhinishwa za Corewell Health NHSC & MSLRP

SERA: Ili kutoa huduma bila malipo na zilizopunguziwa bei kwa wanaohitaji. Wagonjwa wanaopokea huduma katika Corewell Health National Health Service Corps (“NHSC”) au eneo lililoidhinishwa la Michigan State Loan Repayment Program (“MSLRP”) watatathminiwa ili kubaini iwapo watapata usaidizi wa kifedha kulingana na masharti ya NHSC ya mapato na ukubwa wa familia na hawatathminiwa kulingana na vigezo vingine.

MADHUMUNI: Wagonjwa wote wanaotafuta huduma katika sehemu za Corewell Health NHSC & MSLRP wanahakikishiwa kuwa watapewa huduma bila kujali uwezo wao wa kulipa. Hamna atayekataliwa kwa sababu ya kukosa njia za kifedha za kulipa. Mpango huu umebuniwa ili kutoa huduma isiyolipishwa au ambayo bei yake imepunguzwa kwa wale ambao hawana uwezo, au wana uwezo mchache, wa kulipia huduma zao za matibabu (wasio na bima au wenye bima ya kiasi kidogo).

Wagonjwa wanaopokea huduma katika sehemu zilizoidhinishwa za NHSC au MSLRP wanaweza kutumia [Ombi la Faragha la Usaidizi wa Kifedha kwenye NHSC/MSLRP](#). Wanaotuma maombi ambao wanapokea huduma katika maeneo ya NHSC au MSLRP hawatakiwi kutuma ombi la manufaa kutoka kwa bima ya washirika wengine, jimbo, serikali au mipango mingine ya misaada.

Maeneo yaliyoidhinishwa ya Corewell Health NHSC & MSLRP yatakuwa na Mpango wa Punguzo Maalum (Sliding Fee Scale Discount Program) kwa wote ambao hawawezi kulipia huduma zao. Hamna asiyeweza kulipia huduma katika eneo la NHSC au MSLRP atakayezuliwa kupata huduma hizo. Corewell Health itazingatia ustahiki kwenye mpango kulingana na uwezo wa mtu wa kulipa na haitabagua kwa misingi ya mbari, rangi, jinsia, nchi asili, ulemavu, dini, umri, mwelekeo wa ngono au utambulisho wa jinsia ya mtu. Mwongozo wa Serikali wa Kubaini Umaskini (“FPG”) unatumia kubuni na kusasisha kila mwaka ratiba ya kupunguza ada (SFS) ili kubaini ustahiki. Hata hivyo, wagonjwa wanaopokea huduma katika eneo lililoidhinishwa la Corewell Health NHSC au MSLRP ambao wako katika asilimia isiyozidi 250 katika kiwango cha umaskini (angalia <https://aspe.hhs.gov/poverty-guidelines> ili upate mwongozo wa sasa) wataondolewa dhima yote ya kifedha (huduma isiyolipishwa) kwa huduma zinazotolewa katika eneo lililoidhinishwa la NHSC au MSLRP lenye mpango wa kupunguza ada.

UTARATIBU:

Mwongozo ufuatao unapaswa kufuatwa katika Mpango wa Punguzo Maalum.

1. Arifa: Corewell Health itawaarifu wagonjwa kuhusu Mpango wa Punguzo Maalum kupitia:
 - Maelezo ya Sera ya Malipo yatapatikana kwa wagonjwa wote wakati wa huduma.
 - Arifa ya Mpango wa Punguzo Maalum itatolewa kwa kila mgonjwa baada ya kusajiliwa.
 - Maelezo kuhusu upatikanaji wa Mpango wa Punguzo Maalum yatajumuishwa na ilani za ukusanyaji zinazotumwa na Corewell Health.
 - Ufafanuzi wa Mpango wa Punguzo Maalum na fomu yetu ya kutuma ombi, hupatikana kwenye tovuti ya Corewell Health.
 - Corewell Health huweka arifa ya Mpango wa Punguzo Maalum katika eneo la kusubiri la kliniki.
2. Omba punguzo: Maombi ya huduma zilizopunguzwa ada yanaweza kufanywa na wagonjwa, wanafamilia, wafanyakazi wa huduma za jamii au wengine wanaofahamu ugumu uliopo wa kifedha. Mpango wa Punguzo Maalum unapatikana tu kwa wanaotembelea kliniki. Maelezo na fomu zinaweza kupatikana kwenye Dawati ya Usajili na Ofisi ya Biashara.

3. Usimamizi: Utaratibu wa Mpango wa Punguzo Maalum utasimamiwa na timu ya Ukaguzi wa Wagonjwa Wanaoweza Kupata Usaidizi wa Kifedha. Maelezo kuhusu FAP na sera na utaratibu wa Mpango wa Punguzo Maalum yatatolewa kwa wagonjwa. Wafanyakazi wanapaswa kutoa usaidizi wa kujaza fomu ya ombi. Hadhi na usiri zitazingatiwa kwa wote wanaotafuta na/au wanaopewa huduma za afya.
4. Kujaza Fomu ya Ombi: Mgonjwa au mhusika lazima ajaze fomu ya Ombi la Faragha la Usaidizi wa Kifedha kikamilifu kwenye NHSC na MSLRP. Wafanyakazi watapatikana, inavyohitajika, ili kumsaidia mgonjwa au mhusika katika kutuma ombi. Kwa kutia saini kwenye ombi, watu wanathibitisha mapato yao jinsi ilivyobainisha kwenye fomu ya maombi.
5. Ustahiki: Mapunguzo yatalingana na mapato na ukubwa wa familia pekee.
 - a. Familia inafafanuliwa kuwa: kundi la watu wawili au zaidi (ambapo mmoja ni mmiliki wa nyumba) wenye uhusiano wa kuzaliwa, ndoa, au uasili na wanaishi pamoja; watu wote kama hao (wakiwemo wanachama wanaohusiana wa familia ndogo) wanachukuliwa kuwa wanachama wa familia moja. Corewell Health itakubali watu wa familia ambao hawahusiani wakati wa kuhesabu ukubwa wa familia.
 - b. Mapato yanajumuisha: ujira wote; mishahara; bakshishi; mapato kutoka kwa biashara na kujiajiri; malipo ya kutoajiriwa; mapato ya fidia ya wasio na kazi; mapato ya fidia ya wafanyakazi; Bima ya Ustawi wa Jamii; Mapato ya Ziada ya Ustawi; malipo ya wanajeshi waliostaafu; manufaa ya walionusurika; mapato ya pensheni au kustaafu; riba; faida; mirabaha; mapato kutoka kwa nyumba za kukodisha, nyumba, na amana; masurufu; usaidizi wa watoto; usaidizi kutoka nje ya familia; na vyanzo vinginevyo.
6. Uthibitishaji wa mapato: Wanaotuma maombi wanaweza kuwasilisha yafuatayo: W-2 ya mwaka uliopita, hati mpya zaidi za mishahara, barua kutoka kwa mwajiri au Fomu ya 4506-T (iwapo W-2 haijatumwa). Watu ambao wamejiajiri wanaweza kutakiwa kutuma maelezo ya mapato ya miezi mitatu iliyopita na gharama za biashara. Lazima maelezo ya kutosha yawasilishwe ili kubaini ustahiki wa kujiunga kwenye mpango. Utangazaji binafsi wa mapato unaweza kutumiwa. Wagonjwa ambao hawawezi kutoa uthibitishaji ulioandikwa wanaweza kutoa taarifa iliyotiwa sahihi ya mapato.
7. Mapunguzo: Wagonjwa hao walio katika maeneo yaliyoidhinishwa ya NSHC au MSLRP wenye mapato yasiyozidi 250% ya umaskini watapokea punguzo la 100% la huduma za afya (yaani, watapokea huduma bila malipo). Wagonjwa katika maeneo yaliyoidhinishwa ya NHSC & MSLRP wanastahiki kupata punguzo hili kwa siku 90 kuanzia tarehe ya uamuzi na lazima watume ombi jipya kila baada ya siku 90.
8. Arifa ya wanaotuma ombi: Matokeo ya uamuzi wa Mpango wa Punguzo Maalum yatatolewa kwa waliotuma maombi kwa maandishi, au panapohitajika, sababu ya kukataliwa. Maombi ya mpango hushughulikia madeni ya wagonjwa kwa miezi sita kabla ya tarehe ya kutuma ombi na pesa zozote zitakazodaiwa ndani ya siku 90 baada ya tarehe ya kuidhinishwa, isipokuwa hali yao ya kifedha ibadilike kwa kiasi kikubwa. Anayetuma ombi ana chaguo la kutuma ombi tena baada ya siku 90 au wakati wowote ambapo kuna mabadiliko makubwa katika mapato ya familia. Wakati mtu anatuma ombi tena, kipindi cha kukagua kitakuwa chini ya miezi sita au mwisho wa muda wa ombi lake la mwisho.
9. Kukataa Kulipa: Iwapo mgonjwa ataonyesha nia ya kutolipa au anaondoka hospitalini bila kulipia huduma, mgonjwa huyo ataarifiwa kupitia barua kuhusu wajibu wake wa kulipa. Iwapo mgonjwa hajatuma ombi la ratiba ya kupunguza ada, maelezo kuhusu Mpango wa Punguzo Maalum yatajumuishwa pamoja na ilani. Iwapo mgonjwa hatafanya juhudi ya kulipa au atakosa kujibu ndani ya siku 60, hii itachukuliwa kuwa amekataa kulipa. Katika hali hii, Corewell Health inaweza kugundua chaguo, zikiwemo, lakini si tu kumpa mgonjwa mpango wa malipo, kuondoa gharama, au kuelekeza mgonjwa kwa wakusanyaji. Sera ya Malipo na Ukusanyaji kwenye Corewell Health inatumika tu kwa wagonjwa wa NHSC & MSLRP ambao wamezidi 250% ya FPG. Kama ilivyofafanuliwa hapo juu, wale walio chini ya 250% ya FPG hawalipii huduma, kwa hivyo sera ya ukusanyaji haitumiki kwao.

Huluki zitarejelea Hati husika zilizo katika hati hii panapohitajika
Huenda machapisho ya hati hii hayazingatii tarehe na yanayapaswa kuchukuliwa kuwa yasiyodhibitiwa.

10. Kuhifadhi rekodi: Maelezo yanayohusiana na uamuzi wa Mpango wa Punguzo Maalum yatahifadhiwa na msimamizi wa mpango. Maelezo kuhusu kuidhinishwa na kukataliwa kwa maombi yatahifadhiwa kwenye mfumo wa usimamizi na kufuatiliwa na msimamizi wa mpango.
11. Ukaguzi wa sera na utaratibu: SFS itasasishwa kulingana na utaratibu wa sasa wa Mwongozo wa Serikali wa Kubaini Umaskini. Corewell Health pia itakagua mabadiliko yanayoweza kufanywa katika sera na taratibu zetu na kwa ajili ya kutathmini mbinu za taasisi ambazo zinaweza kutumika kama vikwanzo vinavyowazuia wagonjwa wanaostahiki wasipate huduma zetu za jumuiya.
12. Bajeti: Katika mchakato wa kila mwaka wa bajeti, kiasi cha huduma ya Mpango wa Punguzo Maalum kitawekwa katika bajeti kama makato kutoka kwa mapato.

Ratiba ya Kupunguza Ada

Ukubwa wa Familia	MWONGOZO SERIKALI WA KUBAINI UMASKINI	
	100%	250%
1	\$15,060	\$37,650
2	\$20,440	\$51,100
3	\$25,820	\$64,550
4	\$31,200	\$78,000
5	\$36,580	\$91,450
6	\$41,960	\$104,900
7	\$47,340	\$118,350
8	\$52,720	\$131,800
Kila mtu wa ziada	\$5,380	\$13,450

Huluki zitarejelea Hati husika zilizo katika hati hii panapohitajika
Huenda machapisho ya hati hii hayazingatii tarehe na yanayapaswa kuchukuliwa kuwa yasiyodhibitiwa.

Kiambatisho cha C

Ilani ya Kutobagua:

Corewell Health na kampuni zake zote tanzu zinapaswa kutoa huduma bora za afya kwa watu wote, kwa mujibu wa sera yake. Corewell Health haitabagua kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, uraia, jinsia, dini, umri, ulemavu, imani za kisiasa, mwelekeo wa ngono, hali ya ndoa au familia. Maamuzi ya kusajiliwa na matibabu yatalingana kimahususi na mahitaji ya kimatibabu ya mgonjwa na uwezo wa hospitali kutoa huduma za matibabu na za kiafya zinazohitajika. Hutakatazwa kujisajili wala kupata matibabu kwa misingi ya kabila, rangi, ngono, jinsia, mbari, asili ya nchi, dini, ulemavu, umri, hali ya HIV, hali ya uanajeshi, chanzo cha malipo ya huduma au kwa misingi mingine yoyote iliyopigwa marufuku na sheria za serikali, za jimbo au za kimaeneo. Wagonjwa watatibiwa kulingana na utambulisho wa jinsia yao.

Angalia sera ya [Haki na Wajibu wa Wagonjwa](#) (Corewell Health Southeast Michigan), [Haki na Wajibu wa Wagonjwa](#) (Corewell Health Southwest Michigan) au [Haki na Wajibu wa Wagonjwa](#) (Corewell Health West Michigan) ili upate maelezo zaidi.

Corewell Health:

- Hutoa huduma na misaada bila malipo kwa watu walio na ulemavu ili wawasiliane ipasavyo nasi, kama vile:
 - Wakalimani waliohitimu wa lugha ya ishara
 - Maelezo yaliyoandikwa katika miundo mingine (maandishi makubwa, sauti, miundo ya kielektroniki inayoweza kufikiwa, miundo mingine)
- Hutoa huduma za lugha bila malipo kwa watu ambao lugha yao msingi si Kiingereza, kama vile:
 - Wakalimani waliohitimu
 - Maelezo yaliyoandikwa kwa lugha nyingine

Iwapo unahitaji huduma hizi, kwa Corewell Health Southwest and West Michigan wasiliana na Huduma za Lugha mahususi katika: 616.267.9701 or 1.844.359.1607 (TTY:711).

Kwa maeneo ya Corewell Health Southeast wasiliana na Idara ya Huduma za Familia na Wagonjwa katika: 313-593-7070 (Dearborn, Taylor, Trenton, na Wayne), 947-521-8880 (Farmington Hills), 248-551-7040 (Grosse Pointe, Royal Oak, Troy), 248-426-6976 (Farmington Hills RNC), 248-743-9500 (Corewell Health Southeast Michigan Home Health Services). 313-253-9024 (Dearborn RNC) au 947-522-2007 (Corewell Health Southeast Michigan Medical Group).

Iwapo unaamini kuwa Corewell Health imeshindwa kutoa huduma hizi au imebagua kwa njia nyingine kwa misingi ya mbari, rangi, nchi asili, umri, ulemavu, au jinsia, mwelekeo wa ngono, utambulisho wa jinsia au dini, unaweza kutuma malalamiko kupitia:

- Kwa Corewell Health Southeast Michigan
Patient Experience Department
26901 Beaumont Blvd.
Southfield, MI 48033
947-522-1472
Pfcc@beaumont.org
- Kwa Corewell Health Southwest and West Michigan
Director, Patient Experience
100 Michigan St NE MC 006
Grand Rapids, MI 49503
616-391-2624; bila malipo: 1-855-613-2262
patientrelations@corewellhealth.org

Huluki zitarejelea Hati husika zilizo katika hati hii panapohitajika
Huenda machapisho ya hati hii hayazingatii tarehe na yanayapaswa kuchukuliwa kuwa yasiyodhibitiwa.

Unaweza kuwasilisha malalamiko ana kwa ana au kupitia barua, faksi au barua pepe. Iwapo unahitaji usaidizi wa kuwasilisha malalamiko, Msimamizi wa Huduma za Wagonjwa anaweza kukusaidia.

Unaweza pia kuwasilisha malalamiko ya haki za raia kwa Idara ya Huduma za Afya na Binadamu nchini Marekani, Ofisi ya Haki za Raia kwa njia ya kielektroniki kupitia Tovuti ya Ofisi ya Malalamiko ya Haki za Kiraia, inayopatikana kwa <https://ocrportal.hhs.gov/ocr/portal/lobby.jsf>, au kupitia barua pepe au simu kwa:

U.S. Department of Health and Human Services
200 Independence Avenue SW, Room 509F, HHH
Building Washington, DC 20201
1-800-368-1019, 800-537-7697 (TDD).

Fomu za malalamiko zinapatikana katika <http://www.hhs.gov/ocr/office/file/index.html>

Wasiliana Nasi

Español (Spanish)

ATENCIÓN: Si usted habla español, tiene a su disposición servicios gratuitos de asistencia lingüística. Llame al 1-844-359-1607 (TTY: 711).

(Arabic) العربية

ملحوظة: إذا كنت تتحدث اللغة العربية، فإن خدمات المساعدة اللغوية تتوافر لك بالمجان. اتصل برقم 1-844-359-1607 (رقم هاتف الصم والبكم: 711).

中文 (Chinese): 國語/普通話 (Mandarin), 粵語 (Cantonese)

請注意：如果您講中文，您可以獲得免費的語言輔助服務。請撥打1-844-359-1607 (TTY 手語翻譯：711)。

Tiếng Việt (Vietnamese)

CHÚ Ý: Nếu bạn nói Tiếng Việt, có các dịch vụ hỗ trợ ngôn ngữ miễn phí dành cho bạn. Gọi số 1-844-359-1607 (TTY: 711).

Ako govornite srpsko (Serbian, Croatian or Bosnian)

OBAVJEŠTENJE: Ako govornite srpsko-hrvatski, usluge jezičke pomoći dostupne su vam besplatno. Nazovite 1-844-359-1607 (TTY: 711). (TTY- Telefon za osobe sa oštećenim govorom ili sluhom: 711).

አማርኛ (Amharic)

ማስታወሻ: የሚናገሩት ቋንቋ አማርኛ ከሆነ የትርጉም እርዳታ ድርጅቶች፣ በነጻ ሊያግዝዎት ተዘጋጅተዋል። ወደ ሚከተለው ቁጥር ይደውሉ 1-844-359-1607. (ሙስማት ለተሳናቸው: (TTY: 711).

नेपाली (Nepali)

ध्यान दिनुहोस्: तपाईंले नेपाली बोल्नुहुन्छ भने तपाईंको निम्ति भाषा सहायता सेवाहरू निःशुल्क रूपमा उपलब्ध छ । फोन गर्नुहोस् 1-844-359-1607 (टिडिवाइ: (TTY: 711).

Thuɔŋjaŋ (Nilotic – Dinka)

PID KENE: Na ye jam në Thuɔŋjaŋ, ke kuony yenë kɔc waar thook atō kuka lëu yök abac ke cïn wënh cuatë piny. Yuopë 1-844-359-1607 (TTY: 711).

Kiswahili (Swahili)

KUMBUKA: Ikiwa unazungumza Kiswahili, unaweza kupata, huduma za lugha, bila malipo. Piga simu 1-844-359-1607 (TTY: 711).

فارسی (Farsi)

توجه: اگر به زبان فارسی گفتگو می کنید، تسهیلات زبانی بصورت رایگان برای شما فراهم می باشد. با 1.844-359-1607 (TTY: 711). تماس بگیرید.

Français (French)

ATTENTION : Si vous parlez français, des services d'aide linguistique-vous sont proposés gratuitement. Appelez le 1.844-359-1607 (TTY : 711).

မြန်မာ (Burmese)

သတိပြုရန်- သင် မြန်မာစကားပြောဆိုပါက ဘာသာစကား အကူအညီဝန်ဆောင်မှုများကို အခမဲ့ ရရှိနိုင်ပါသည်။ 1-844-359-1607, (TTY: 711) ကို ခေါ်ဆိုပါ။

فارسی دری (Dari)

توجه اگر به زبان دری صحبت می کنید، خدمات کمک زبانی بصورت رایگان برای شما در دسترس است. تماس با 1.844-359-1607 (TTY: 711).

Kreyòl Ayisyen (Haitian Creole)

ATANSYON: Si ou pale Kreyòl Ayisyen, gen èd nan lang ki disponib gratis pou ou. Rele nimewo 1-844-359-1607 (TTY: 711).

Ikinyarwanda (Kinyarwanda)

ICYITONDERWA: Niba uvuga ikinyarwanda, serivisi z'ubufasha ku byerekeye ururimi, urazihabwa, ku buntu. Hamagara 1-844-359-1607 (ABAFITE UBUMUGA BW'AMATWI BIFASHISHA ICYUMA CYANDIKA -TTY: 711).

Soomaali (Somali)

DIGTOONI: Haddii aad hadasho Soomaali, adeegyada caawimada luqadda, oo bilaasha, ayaad heli kartaa. Wac 1.844-359-1607 (TTY: 711).

اللهجة السودانية (Sudanese)

ملحوظة: إذا كنت تتحدث اللهجة السودانية، فإن خدمات المساعدة اللغوية تتوافر لك بالمجان. اتصل على الرقم 1-844-359-1607 (رقم الصم والبكم: 711).

தமிழ் (Tamil)

கவனம்: நீங்கள் தமிழ் பேசினால், உங்களுக்கு இலவசமான மொழி உதவிச் சேவைகள் கிடைக்கின்றன. இந்த எண்ணை அழைக்கவும்: 1-844-359-1607 (TTY: 711).

ትግርኛ (Tigrinya)

ትኹረት: ትግርኛ እንደሕገ ትዘረብ ከንካ፣ ናይ ቋንቋ ደገፍ ኣልግሎታት፣ ብናጻ ክቕርቡልካ እዮም። ደውል 1.844-359-1607 (TTY: 711)።